Magufuli

Harmonize

Mmmmh
I wish ningemwona Magufuli
Nipige magoti
Nimpongeze hadharani

Yaani Rais wa muungano wa Jamhuri
Mchapakazi hachoki
Anaye pinga nani?

Mmmh,
Ametuvusha vikwazo
Wewe nami ona nchi anavyoijenga
Flyover sa tunazo, daraja kigamboni
Airport imesha jengwa

Acha nikupongeze Kwa Air Tanzania (Ielewe)
Zidi baba tuongeze Airbus Bombardier (Ielewe)
Standard gauge tuteleze Kusafiri unasinzia (Ielewe)
Acheni tu niwaeleze Magufuli papa nia (Ielewe)

Oooh dady
Magufuli Cheza nikuone (Kwangwaru)
Wasopenda wabane choo (Kwangwaru)
Magu muacheni (Kwangwaru)

Oooh daddy
Asa Cheza nikuone (Kwangwaru)
Jembe toka chato (Kwangwaru)
Magufuli ndo Rais wa wanyonge (Kwangwaru)

Aga, mpole mtu wa dini
Hajachoka tunashukuru
Amesamehe mara sabini
Papi Kocha sa yuko huru

Wa-Tanzania tupewe nini?
Vilokufa yeye kavifufua
Karudisha nidhamu serekalini
Ukileta njanja anatumbua EEh!

Sekta ya madini
Umeme maji kero zimepungua (Asa wee)
Elimu bure vijijini Watoto shule wanabukua (Asa wee)
Ifikapo elfu mbili na ishirini Kura yangu chukua (Asa wee)
Asa tufiche ya nini 'Magu' uongozi anaujua (Asa wee)

Dar es Salaam mwendo kasi Vituo vya afya kila kata (Ielewe)
Machinga tunachapa kazi Tena huru bila shaka (Ielewe)
Borigi utani ameongeza Uchumi uweze panda (Ielewe)
Serekali Dodoma inapendeza Tanzania ya viwanda (Ielewe)

Oooh daddy
Magufuli Cheza nikuone (Kwangwaru)
Wasopenda wabane choo (Kwangwaru)
Magu muacheni (Kwangwaru)

Oooh daddy

Asa cheza nikuone (Kwangwaru)
Jembe toka chato (Kwangwaru)
Magufuli ndo Rais wa wanyonge (Kwangwaru)

Asa wote wa-Tanzania
Tusimame imara (Imara imara)
Yaani wote Tanzania
Imara Tanzania tusonge mbele

John Pombe Magufuli
Simama imara (Imara imara)
Yaani wote tusonge mbele
Imara Tanzania tusonge mbele

Oooh mama Samia Suluhu
Basi simama imara (Imara imara)
Kwa pamoja tusonge mbele
Imara Tanzania tusonge mbele

Baba Kassim Majaliwa
Simama imara (Imara imara)
Kwa pamoja tusonge mbele
Imara Tanzania tusonge mbele

Wasafi Records

Sponzor: www.srovnavac.cz - vyberte si pojištění online!